ISO 9001:2015 Certified

# The Regulator

Linatolewa bure

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISSN: 0856 - 8030 NA. 3/2024 JULAI - SEPTEMBA 2024



## Tanzania yapunguza tofauti mawasiliano kidijiti

**Ni miongoni mwa nchi 25 ulimwenguni kwa usalama mitandaoni**

## Kuenea, laini za simu za mkononi miongoni mwa watu mikoani (idadi ya watu kwa mujibu wa sensa ya Agosti 2022)

| Na. | Mkoa | Idadi ya watu | Laini | Asilimia kuenea | Nafasi kitaifa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dar es Salaam | 5,382,728 | 14,848,400 | 275.9 | 1 |
| 2 | Arusha | 2,356,255 | 4,856,040 | 206 | 2 |
| 3 | Mbeya | 2,343,754 | 4,641,245 | 198 | 3 |
| 4 | Kilimanjaro | 1,861,934 | 3,112,150 | 167.14 | 4 |
| 5 | Njombe | 889,946 | 1,418,991 | 159.4 | 5 |
| 6 | Iringa | 1,192,728 | 1,882,680 | 157.84 | 6 |
| 7 | Mwanza | 3,699,872 | 5,344,286 | 144.44 | 7 |
| 8 | Dodoma | 3,085,625 | 4,306.681 | 139.57 | 8 |
| 9 | Mtwara | 1,634,947 | 2,241,081 | 137.07 | 9 |
| 10 | Pwani | 2,024,947 | 2,650,049 | 130.87 | 10 |
| 11 | Morogoro | 3,197,104 | 4.054,475 | 126.81 | 11 |
| 12 | Lindi | 1,194,028 | 1,401,899 | 117.40 | 12 |
| 13 | Songwe | 1,344,687 | 1,565.199 | 116.39 | 13 |
| 14 | Ruvuma | 1,848,794 | 2,128,442 | 115.125 | 14 |
| 15 | Tabora | 3,391,679 | 3,901.131 | 115.02 | 15 |
| 16 | Tanga | 2,615,597 | 2,976,829 | 113.81 | 16 |
| 17 | Manyara | 1,892,502 | 2,016,981 | 106.577 | 17 |
| 18 | Shinyanga | 2,241,299 | 2,188, 037 | 97.62 | 18 |
| 19 | Singida | 2,008,058 | 1,876,065 | 93.426 | 19 |
| 20 | Geita | 2,977,608 | 2,689,821 | 90.334 | 20 |
| 21 | Simiyu | 2,140,497 | 1,854,006 | 86.002 | 21 |
| 22 | Rukwa | 1,540,519 | 1,324,883 | 81.619 | 22 |
| 23 | Mara | 2,372,015 | 2,010,307 | 84.75 | 23 |
| 24 | Katavi | 1,152,958 | 833,849 | 72.322 | 24 |
| 25 | Kagera | 2,989,299 | 1,985,015 | 66.40 | 25 |
| 26 | Kigoma | 2,470,967 | 1,609,777 | 65.147 | 26 |
| 27 | Mjini Magharibi | 893,169 | 510.853 | 57.195 | 27 |
| 28 | Kusini Unguja | 195,873 | 110,970 | 56.65 | 28 |
| 29 | Kaskazini Pemba | 272,091 | 124,684 | 45.82 | 29 |
| 30 | Kusini Pemba | 271,350 | 124,472 | 45.87 | 30 |
| 31 | Kaskazini Unguja | 257,290 | 73,743 | 28.66 | 31 |

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
Na. 1/2024-2025. JULAI - SEPTEMBA, 2024

# The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## Sheria Na. 12 ya mwaka 2003 iliyoianzisha TCRA inaipa Mamlaka wajibu katika majukumu yafuatayo:

1. Kukuza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda maslahi ya watumiaji;
3. Kulinda mitaji ya Watoa Huduma wenye ufanisi;
4. Kukuza upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa kwa watumiaji wote wakiwamo wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio na walioko katika mazingira magumu;
5. Kuimarisha Elimu kwa Umma, uelewa na ufahamu wa huduma zinazosimamiwa na TCRA, ikiwa ni pamoja na:
   (i) Haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazosimamiwa;
   (ii) Namna ya kuwasilisha malalamiko na migogoro na utaratibu wa utatuzi wake; na
   (iii) Kazi na majukumu ya Mamlaka kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

## MKAKATI WA TCRA 2021/22-2025/26 NA MALENGO YA KIMKAKATI

Mamlaka imeandaa Malengo mbalimbali ili kufikia maono yake katika kukabiliana na mambo muhimu kama yalivyobainishwa katika uchambuzi wa hali halisi ya kisekta. Malengo hayo ni:-

1. Kukuza miundombinu na huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta yenye usalama, ufanisi na imara;
2. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta zenye ubora na unafuu;
3. Kuimarisha ubunifu wa huduma zinazodhibitiwa, uandaaji wa maudhui ya ndani na ujanibishaji;
4. Kuimarisha ufanisi wa huduma zinazodhibitiwa na kuwalinda wadau; na
5. Kuimarisha uwezo wa taasisi.

## MATOKEO YA MKAKATI

1. Kupatikana kwa huduma za mawasiliano za uhakika na salama;
2. Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu;
3. Jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani;
4. Kukua kwa ufanisi wa sekta ya mawasiliano na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo, kanuni ndogo na viwango kwa wadau wa sekta ya mawasiliano; na
5. Kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji wa taasisi.

## SERA YA UBORA

Kutokana na nguvu za kisheria za kusimamia sekta za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta Tanzania, TCRA imejidhatiti kuweka mazingira mazuri kwa Wenye Leseni kwa kutoa rasilimali, kudumisha na kuendelea kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Ubora ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na nafuu kwa watumiaji ili kukidhi matakwa ya Sheria na ya kiudhibiti.

## BODI YA WAHARIRI

**Mwenyekiti**
Mhandisi. Mwesigwa Felician

**Katibu**
Bw. Rolf Kibaja

**Wajumbe**
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

**Anwani ya ofisi za uhariri**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz;
dg@tcra.go.tz
@tcra_tanzania

# Yaliyomo

04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu




13 Hatari za kumsajilia mtu laini ya simu



Mapya kwenye sheria

06 Tanzania inavyoondoa tofauti mawasiliano




Makala kuu

15 TCRA yapongezwa kufanikisha teknolojia wezeshi




Mwongozo wa watumiaji

10 Tanzania juu duniani viwango vya usalama mitandaoni




20 Takwimu sekta ya Mawasiliano



BARUA YA MHARIRI

# Tanzania yapunguza tofauti mawasiliano kidijiti

Makala kuu ya toleo hili inaeleza namna Tanzania ilivyofikia hatua muhimu kwenye juhudi zake kuondoa tofauti kwenye mawasiliano.

Imepunguza tofauti katika kuenea kwa huduma za mawasiliano miongoni mwa watu, kijiografia na kwenye uwezo wa kumiliki na kutumia vifaa vya kielektroniki.

Tumenukuu Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) na namna linavyoipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mchango wake kwenye mafanikio haya.

Kama sehemu ya majukumu yake ya kuendeleza sekta ya mawasiliano nchini, TCRA inatekeleza mipango ya kuinua viwango vya ustadi wa wananchi, hususan wanafunzi, kwenye masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na ya kidijiti. Wanafunzi watatu waliofadhiliwa na TCRA wameibuka kidedea kwenye mashindano ya hisabati Afrika  Agosti mwaka huu.

Tuna ripoti ya ushindi wa Tanzania kimataifa kwenye ufanisi matumizi ya intaneti. Kwa mujibu wa Fahirisi ya Usalama Mtandaoni Ulimwenguni ya mwaka 2023 iliyotolewa Septemba mwaka huu,Tanzania imeshika nafasi ya 10 kati ya nchi 46 zilizopewa hadhi ya ngazi ya juu na kuwekwa kundi la mifano bora katika usimamizi wa usalama mtandaoni.

Mwitikio wa uhamasishaji unaofanywa na TCRA kuhusu masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati umekuwa mzuri. Wanafunzi watatu wa Tanzania waliofadhiliwa na TCRA wameshinda medali kwenye mashindano ya hisabati kwa shule za sekondari Afrika.



Takwimu za mawasiliano za kila robo mwaka zinaonesha kukua kwa huduma na miundombinu kwenye sekta za mawasiliano ya simu, intaneti na utangazaji.

Kuna makala kuhusu mwelekeo wa huduma za posta baada ya kuongezeka kwa vitu vinavyosafirishwa kimataifa.

---




Jarida hili linakuwezesha kupitia na kupata stadi mpya na pia kupanua mtandao wako wa watu wenye weledi kama wewe. Kupata nakala za bure za jarida hili na kuwasilisha maoni, tuma barua pepe kwa

regulator.magazine@tcra.go.tz | barua@tcra.go.tz

Soma kujisajili

Tunakaribisha maoni na hoja kutoka kwa wasomaji wetu. Kwa maelezo zaidi tafadhali piga simu ya bure kwenye namba ya wateja wa TCRA, ambayo ni **0800008272.**

UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

# Maendeleo ya teknolojia na uchumi wa kidijiti



Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

*(Ujumbe huu unatokana na wasilisho la Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari kwa wadau Septemba 2024. Tumefupisha na kuuandaa kwa matumizi ya jarida hili.)*

Kihistoria, dunia imepitia mabadiliko mengi ya kiteknolojia. Kulikuwa na enzi za matumizi ya zana za mawe, chuma na ujio wa viwanda; na sasa tuko kwenye enzi ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, ambayo inawezesha uchumi wa kidijiti.

Teknolojia ya habari inahusisha vitu vingi. Hivi ni pamoja na matumizi ya kompyuta, kuhifadhi, mifumo na vitu vingi na michakato mbalimbali kuunda, kuchakata, kuhifadhi, kulinda na kubadilishana data za kielektroniki.

Tunaona mabadiliko mengi ya kiteknolojia, hasa sayansi ya kompyuta, mawasiliano ya simu, sayansi ya data na teknolojia zinazowezesha shughuli za kifedha.

Kuna misamiati mikubwa kama vile mifumo ya kuhifadhi kumbukumbu za shughuli ziliyofanyika kwenye kompyuta mbalimbali zilizounganishwa kuwezesha matumizi ya wahusika wenye aina moja ya matumizi. Pia tunaona kuwepo kwa akili mnemba, kwa kifupi AI.

Wakati mwingine watu wanapozungumzia akili mnemba ni kama vile wanasahau kuwa AI inatengenezwa na akili ya binadamu na kwamba inabidi iandaliwe.

AI imetokana na maendeleo ya teknolojia ya kompyuta na ni hatua ya juu zaidi ya mifumo ya kompyuta na programu wezeshi. Ni nadharia ya kuandaa na kutumia mifumo ya kompyuta inayoweza kufanya kazi zinazohitaji akili na binadamu bila kutegemea binadamu moja kwa moja.

Vitu vinavyofanywa na AI inabidi viandaliwe kufanya kazi kama binadamu. Teknolojia hii ni changamani kwa kuwa inahusisha kanuni au maelekezo ya kimahesabu ambayo yakifuatwa na kompyuta kuwepo hali ambapo mifumo inaanza kufanya kazi kama binadamu.

Mabadiliko ya teknolojia ni mtambuka. Mipango kwenye kilimo, miundombinu ya usafiri, uchimbaji madini, elimu na afya kwa mfano inabidi kutekeleza viwango vya utayari wa kutumia mifumo ya kidijiti.

Teknolojia imebadilisha kwa haraka sekta ya fedha. Zamani wateja wa benki walitumia vijitabu vidogo vya akiba na ilibidi wapange foleni kabla ya kupata huduma.



Uhakiki wa akaunti ya mhusika na kuwezesha fedha kutolewa kulichukua angalau saa moja.

**TAARIFA KWA KASI**

Teknolojia imewezesha ubadilishanaji wa taarifa kwa kasi. Hivi sasa kuna mashine za kutoa fedha –ATM. Hizi ni kama kompyuta. Unapoingiza kadi yako, unaanzisha mjadala wa kidijiti kuhusu akaunti yako. Unapewa taarifa za aina mbalimbali kwenye ATM.

Vilevile kuna teknolojia inayowezesha kila kitu kuwasiliana. Hii inaitwa teknolojia wezeshi ya vifaa kuwasiliana kupitia intaneti. Kifupisho chake ni IoT.

IOT inawezesha friji au jokofu kutambua kwamba vitu vya matumizi ndani yake vimepungua au kumalizika. Hivyo kuagiza moja kwa moja kwenye duka la kisasa. Friji itawasiliana na akaunti yako kujua salio na kukujulisha. Unapoamua kulipa na kukamilisha muamala vitu vinapelekwa ilipo friji.

Mifano mingine kwenye uchumi wa kidijiti ni pamoja na teknolojia inayowezesha usafiri wa teksi kwa ufanisi. Hii ni pamoja na Uber na Bolt; huduma ambazo zinawezeshwa na intaneti.

**5G**

Ujio wa uzao wa tano wa teknolojia ya mawasiliano ya vifaa vya mkononi ya kasi,yaani 5G pia umewezesha huduma nyingi zinazohitaji usafirishaji wa data kwa kasi.

Kazi za kidijiti za siku zijazo zitahitaji wataalamu wenye ujuzi na stadi za kuandaa program za kompyuta. Hawa ni pamoja na mabingwa wa hisabati na wa mifumo ya kuchambua data mitandaoni.

TCRA inahamasisha masomo yanayowezesha ustadi na umahiri wa kumudu teknolojia za kidijiti. Masomo hayo ni sayansi, teknolojia, uhandishi na hisabati.

TCRA pia inahimiza uanzishaji wa vilabu vya kidijiti katika ngazi zote za elimu kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu. Lengo ni kuwezesha uelewa wa masomo wezeshi kidjiti kutoka ngazi ya chini ili kufanikisha kuenea masomo yanayowezesha mifumo ya kidijiti ngazi zote.

Tunahitaji mabingwa wa hisabati watakaotuwezesha kupata wahandisi zaidi na kuisaidia Tanzania kujenga na kuimarisha kikamilifu uchumi wa kidijiti.



MAKALA KUU

# Tanzania inavyoondoa tofauti mawasiliano

## Tanzania yapunguza tofauti mawasiliano kidijiti

Taifa limefikia hatua muhimu kwenye juhudi zake za kuondoa tofauti kwenye mawasiliano na ripoti za hivi karibuni zinaonesha inaongoza Afrika Mashariki kwenye maeneo muhimu na wezeshi.

Imepunguza tofauti katika kuenea kwa huduma za mawasiliano miongoni mwa watu, kijiografia na kwenye uwezo wa kumilki na kutumia vifaa vya kielektroniki.

Tofauti za kwenye mawasiliano zinatokana na kutokuwa na usawa kwenye upatikanaji, kuchukuliwa kwa matumizi na kutumika teknolojia za habari na mawasiliano (TEHAMA) na huduma kati ya maeneo na miongoni mwa watu.

Vilevile zinahusu kutokuwepo usawa kwenye uchukuaji kwa matumizi ndani ya maeneo na makundi ya watu.

Sera dhaifu na mifumo ya usimamizi isiyokidhi matarajio, miundombinu hafifu, viwango vya chini vya uelewa wa masuala ya kidijiti, uvumbuzi kidogo na tofauti za kijinsia vinakwamisha azma za nchi kueneza huduma za mawasiliano kwa wote.

Mipango inayosukuma kutumika TEHAMA na juhudi za pamoja zinazoleta tija zaidi miongoni mwa wadau wa TEHAMA vinawezesha nchi kupunguza tofauti za mawasiliano kidijiti. Mipango thabiti ya kutumia kikamilifu raslimali adimu pia inachangia.

Ripoti mbalimbali zinaonesha namna Tanzania inavyokabili tofauti za matumizi ya mawasiliano.

Hizo ni ripoti ya ya mwaka 2024 ya Umoja wa Mawasiliano Afrika Mashariki (EACO), yenye makao yake makuu Kigali Rwanda, andiko la Shirika la Mawasiliano ya Simu Ulimwenguni (ITU) na taasisi ya GSMA ambayo inasimamia maslahi ya watoa huduma za simu za mkononi duniani.

Durusi zinaonesha kuwa mipango ya kuweka miundombinu mipya peke yake haziwezi kuondoa tofauti za mawasiliano kidijiti. Inatakiwa itekelezwe sambamba na kuwezesha uchukuliwaji kwa matumizi na utumiaji wa huduma zinazowezeshwa na teknolojia zilizosimikwa.



Tanzania inazo sera imara na mfumo makini wa usimamizi wenye mwelekeo sahihi. Imeboresha kuenea kwa TEHAMA miongoni mwa watu na maeneo mengi nchini.

Ripoti ya EACO kuhusu sekta ya mawasiliano Afrika mwaka 2023, iliyozinduliwa tarehe 24 Juni 2024 inaonesha kuwa simu za mkononi zimeenea miongoni mwa watu Tanzania kwa asilimia 112. Hii ni juu ya wastani wa Afrika Mashariki wa asilimia 100 na wa Afrika wa asilimia 92.

Ripoti inaonesha pia kwamba Tanzania ina kiwango cha juu zaidi cha kuenea kijiografia kwa simu za mkononi uzao wa pili (2G) Afrika Mashariki. Ni asilimia 92, sawa na wastani wa asilimia 92 kwa eneo hilo.

Vilevile inaongoza kwa kuenea uzao wa nne (4G), ukiwa asilimia 70.2 kulinganisha na asilimia 62 mtawalia. Huu unawezesha intaneti ya kasi.

Uzao wa tano (5G) ulienea kijiografia Tanzania kwa asilimia 2.2 Septemba 2024.

Kwa mujibu wa takwimu za robo mwaka zilizotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Septemba 2024 laini zilizotumika kupata huduma za intaneti Tanzania zilikuwa 41,376,545. Kati ya hizi, asilimia 99.7 zilitumia teknolojia inayowezesha intaneti ya kasi.

Kuenea intaneti miongoni kwa watu kwenye nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuliongezeka kutoka asilimia 49 mwaka 2022 hadi 51 mwaka 2023. Kwa Tanzania kuenea kulitoka asilimia 51 hadi 58 kipindi hicho.

Huduma za pesa kwa simu za mkononi zimechangia kuongezeka matumizi ya simu kwa kuwezesha huduma za kifedha zinazotegemea simu, ripoti ya EACO imeeleza. Akaunti za pesa kwa simu za mkononi Tanzania ziliongezeka kwa asilimia 135 kati ya Desemba 2019 na Septemba 2024.

### Akaunti za pesa kwa simu za mkononi

| Desemba 2019 | | Septemba 2024 |
|---|---|---|
| 25,864,318 | 115% | 60,815,533 |

Taarifa hiyo imeeleza kuwa kuenea kwa akaunti hizo kunatokana na uwekezaji unaoendelea Tanzania ambako miundombinu inajengwa kufikisha na kueneza huduma vijijini.

Tanzania inajenga minara mipya simu za mkononi na kuboresha minara vijijini chini ya mradi uliozinduliwa 2023. Ujenzi na uboreshaji unahusisha zaidi ya minara 1,655 Tanzania nzima. (Rejea makala ukurasa. 11).

Kuna uwiano katika ujenzi wa minara mipya na kuiboresha iliyopo ili itoe huduma kupitia teknolojia ya juu zaidi. Kwa mfano takwimu za TCRA za Juni 2024 zinaonesha kuwa kila mkoa una angalau minara miwili yenye vifaa vinavyowezesha uzao wa tano (5G).

Miundombinu inayoendelezwa ni pamoja na mkongo wa taifa wa mawasiliano ya kasi (NICTBB) ambao unalenmga kuunganisha kata zote 3,956 Tanzania ifikapo 2026. Hii ni sehemu ya mkakati wa kueneza intaneti kwa angalau asilimia 80 ya watu ifikapo 2025.

Waya wa faiba utawekwa kilometa 86,000 zaidi ifikapo 2026.

Tanzania inahimiza uchangiaji wa miundombinu ya mawasiliano.

Ripoti ya hivi karibuni ya kimataifa inaonesha kuwa uchangiaji minada unawezesha kuongezeka watumiaji wa intaneti ya kasi kwa asilimia 14.63. Hii inachangia kukua kwa pato la taifa kwa asilimia 4.8 ndani ya miaka minane.

Hatua za pamoja zinazochukuliwa na wadau kwenye sekta mbalimbali pia zinachangia kupunguza tofauti za mawasiliano kidijiti. Ushiriki wa taasisi zilizo kwenye mlo-longo wa utoaji huduma za kidijiti unaopunguza gharama za kuweka miundombinu na kuiendesha.

Kwa mfano, serikali imepunguza gharama za kupitisha miundombinu kwenye hifadhi ya barabara kutoka ada ya awali na ya kila mwaka ya dola za Kimarekani 1,000 hadi 100, mtawalia.

Ada hizi zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Gharama za maongezi kwenye mtandao wa mtumiaji zilishuka kutoka shilingi 149 kwa dakika mwaka 2019 hadi shilingi 26 Juni 2024.

Gharama kwenda mitandao mingine zilishuka kutoka shilingi 189 kwa dakika hadi shilingi 28. Kiwango cha kila mwaka cha ukuaji wa simu za maongezi kwenda mitandao mingine kilikuwa mara saba ya kile cha simu za ndani ya mtandao wa mtumiaji kati ya mwaka 2019 na 2023.

Wakati simu ndani ya mtandao ziliongezeka kwa asilimia tisa (9) kwa mwaka kipindi hicho, simu za watumiaji kwenda mitandao mingine zilipaa kwa asilimia 61.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari ameeleza kuwa kushuka kwa gharama kwenda mitandao mingine kumesababishwa na kuchangiwa na kupunguzwa kwa gharama za kuunganisha simu baina ya mitandao kipindi hicho. Gharama za kuunganisha zimeshuka kutoka shilingi 15.6 Januari 2018 hadi 1.76 Januari 2024.

| 2018 | | 2024 |
|---|---|---|
| 15.6 Shilingi | 11% | 1.76 Shilingi |

Taarifa ya GSMA inasema ingawaje bei za simu za mkononi Tanzania ni chini kulinganisha na nchi nyingine Afrika, bado ni vigumu watu wengi kumudu simu janja, na zinakula kiasi kikubwa cha vipato.

Wanawake wanaathirika zaidi kwani wengi wana vipato vidogo.

MiIradi ya kupelekea umeme vijijini imeondoa matatizo ya nishati kwa ajili ya televisheni, ving'amuzi na vifaa vingine vya TEHAMA. Hii ni pamoja na kuchajia simu. Umeme wa uhakika pia unawezesha watumiaji kutumia vifaa vya kisasa zaidi kiteknolojia.

Hadi Machi 2024, asilimia 96.4 ya vijiji Tanzania Bara vilikuwa na umeme, kwa mujibu wa Wizara ya Nishati.

Takwimu za TCRA zinaonyesha kuwa Watanzania wengi zaidi wanaachana na simu za kawaida na wanatumia simu zenye uwezo mkubwa, maarufu kama simu janja, ambazo zilienea kwa asilimia 32.6 Machi 2024.

Kupungua gharama za mawasiliano pia kunachangia kupunguza tofauti kidijiti. Wastani wa gharama za maongezi kwenye mtandao wa mtumiaji na kwenda mitandao mingine zilianza kukaribiana mwaka 2020 kufuatia kushuka kidogo kidogo miaka iliyotangulia. Mipango ya watoa huduma na wadau wengine kutoa mikopo ya simu janja imechangia kuongezeka kwake, ingawaje kuna mala-lamiko kuhusu masharti ya baadhi ya mikopo.

Tanzania inatekeleza mipango kadhaa ya kuendelea wanawake katika TEHAMA. Hii ni pamoja na kuwahimiza wanafunzi wasichana kuchukua masomo yanayowezesha stadi za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STUH/STEM).

TCRA imeanzisha mipango ya kueneza TEHAMA kwenye shule na vyuo kwa kuhimiza uanzishaji klabu za kidijiti kwenye ngazi zote za masomo.

Vievile inaendeleza uvumbuzi kwa kutoa raslimali za mawasiliano bure na kwa muda maalum kwa wajasiriamali na wavumbuzi wanaojitokeza ili wajajaribu miradi yao ya kuende-leza matumizi ya mawasiliano ya Tanzania.

TCRA pia inashirikiana na wadau wengine wenye majukumu yanayofanana na yanayochanghia kuelea kwa mawasiliano ya kidiijiti.

Ushirikiano huu umepongezwa na Shirika la Mawasiliano ya Siimu Ulimwenguni (ITU).



## Rejea


1. https://www.thecable.ng/closing-the-digital-divide-in-africa-unfolding-challenges-strategies-and-successstories/
2. Africa's Digital Transformation: Closing the Digital Divide By Kendra L. Gaither. https://carnegieendowment.org/research/2022/04/to-close-africas-digital-divide-policy-must-address-the-usage-gap?lang=en
3. What is the digital divide in Africa? https://typeset.io/questions/what-is-the-digital-divide-in-africa-21b06x0q2y
4. Timothy Laku, Six factors contributing to the digital divide and why policy is urgently needed to close the gap.https://www.timothylaku.com/post/six-factors-contributing-to-the-digital-divide-and-why-policy-is-urgentlyneeded-to-close-the-gap
5. East African Communications Organization (EACO). The 2023 Regional Communications Sector Report, released on Jun 27, 2024. Available on https://ipris.digital/the-2023-eaco-communications-sector-regional-report.
6. International Telecommunication Union (ITU). Tanzania – A solid base for moving to G5 regulation. Published on https://www.itu.int/en/ITU-D/Conferences/GSR/2021/Documents/Publications/Collaborative-Regulation_Case StudyTanzania_Final E.pdf.UNDP Bridging
7. Zanzibar's Digital Divide: A Leap Towards an Inclusive and Sustainable Tomorrow. https://www.undp.org/tanzania/blog/bridging-zanzibars-digital-divide-leap-towards-inclusive-and-sustainable-tomorrow
8. GSMA. Matt Shanahan. Senior Insights Manager, Connected Society. https://www.gsma.com/solutions-andimpact/connectivity-for-good/mobile-for-development/blog/despite-improvements-sub-saharan-africa-hasthe-widest-usage-and-coverage-gaps-worldwide/
9. Determinants of Digital Divide in Africa and Policy Implications. Stephen Kwamena Aikins https://www.igi-global.com/article/determinants-of-digital-divide-in-africa-and-policy-implications/217717.


---

**MATUKIO**

## Wafadhiliwa wa TCRA wavuna medali nne umahiri hisabati Afrika

Wanafunzi watatu wa sekondari waliofadhiliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kushiriki mashindano ya Hisabati Afrika Agosti mwaka huu Afrika Kusini wameshinda medali za shaba, ikiwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kupata heshima hiyo.

Walioshinda ni Ambrose George Rutashobya wa shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga, Zakaria Mataiga Mwita wa Azania na Stella Ludan Maliti wa Sekondari ya Wasichana ya Marian.

Stella alishinda medali mbili na pia alitangazwa "Malkia wa Hisabati".

Wanafunzi watano wa Tanzania walishiriki mashindano hao. Wengine ni Ilham Abdalla Awadhi wa Feza, Zanzibar na Mwanaarab Said Mbwana wa Sekondari ya Lumumba, Zanzibar.

Tanzania ilikuwa ya 15 kati ya nchi washiriki 27 huku Morocco ikiwa ya kwanza.

Mashindano ya hisabati Afrika yanaratibiwa Tanzania na Chama cha Hisabati Tanzania (MAT/CHAHITA), chenye makao makuu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kufuatia ushindi huo, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dkt. Jabiri Bakari amesema Mamlaka hiyo itafadhili masomo yao kwa kuwalipia gharama zote za elimu.

Ameeleza kuwa hii ni sehemu ya juhudi za TCRA kuhamasisha wanafunzi wengi zaidi kupenda masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STUH/STEM).

INTANETI

# Tanzania juu duniani viwango vya usalama mitandaoni

Na Mwandishi wetu

**Tanzania ni ya kwanza Afrika Mashariki na Kati na ni miongoni mwa nchi 46 zinazoongoza ulimwenguni kwa ufanisi kwenye usalama mitandaoni, kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa hivi karibuni na Shirika la Mawasiliano ya Simu Ulimwenguni (ITU).**

Fahirisi ya Usalama Mtandaoni Ulimwenguni ya mwaka 2023 iliyotolewa Septemba mwaka huu na ITU inaonesha kwamba nchi hizo 25 zimethibitisha kujipambanua kwenye masuala ya usalama mitandaoni.

Tanzania imeshika nafasi ya 10 kati ya nchi 46 zilizopewa hadhi ya ngazi ya juu na kuwekwa kundi la mifano bora katika usimamizi wa usalama mtandaoni.

Nchi hizo, ambazo tano ikiwemo Tanzania ni za Afrika, zimetambuliwa kwa maboresho yaliyofanyika kwenye usimamizi wa usalama mitandaoni tangu fahirisi ya mwisho ilipotolewa mwaka 2021.

Fahirisi ya 2024 inaziweka nchi hizo 46 katika nafasi ya juu zaidi kwa mafanikio. Pamoja na tano za Afrika, ziko mbili za Amerika, 20 za Ulaya, 11 za eneo ya Asia na Pasifiki na nane za Kiarabu.

| | | |
|---|---|---|
| **20** Ulaya | **11** Asia | **8** Uarabuni |
| **5** Afrika | **2** Amerika | |

Nchi kadhaa zilizoendelea, kama vile Ubelgiji na Ujerumani hazimo kwenye kundi hili.

ITU – taasisi ya Umoja wa Mataifa inayosimamia TEHAMA, ilianza mpango wa fahirisi hiyo mwaka 2015. Inaitwa GCI, kifupisho cha jina lake kwa Kiingereza.

Tanzania imepanda viwango kwa pointi tisa kwenye nafasi yake Afrika na kwa pointi tatu Afrika Mashariki ndani ya miaka tisa. Ilikuwa ya nne na 12 mtawalia mwaka 2015.

Fahirisi hiyo ni matokeo ya tathmini ya ufanisi katika kusimamia nguzo tano ya usalama mitandaoni.

**Jedwali 1: Nafasi ya Tanzania kwenye GCI kati ya 2015 na 2024 (2023)**

| Mwaka | Afrika Mashariki | Nafasi Afrika |
|---|---|---|
| 2015 | 4 | 12 |
| 2017 | 4 | 11 |
| 2018 | 3 | 6 |
| 2021 | 2 | 4 |
| 2024 | 1 | 3 |

Nguzo tano zinazopimwa kwenye fahirisi hiyo ni sheria na Ujenzi wa uwezo katika masuala ya usalama. Nyingine ni mipango na mikakati ya kiufundi, mfumo wa usimamizi na uendeshaji pamoja na ushirikiano wa ndani ya nchi, kikanda na kimataifa.

Katibu Mkuu wa ITU, Bi. Doreen Bogdan-Martin anaeleza kuwa wanatumia nguzo hizo kwa kuwa usalama mtandaoni ni mtambuka na unagusa sekta nyingi.

Hatua za kisheria zinahusu sheria na kanuni kuhusu makosa na usalama mtandaoni. Tanzania ni mojawapo ya nchi zenye sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi.

Hatua za kiufundi zinajumuisha uwezo katika eneo hili kupitia wakala au taasisi mahsusi za ufundi kwenye nchi husika. Zinahusu pia uwepo wa taasisi za kiufundi na mifumo na utaratibu wa kushughulikia usalama mitandaoni. Taasisi hizi zinaweza kuwa zilizoanzishwa au kuidhinishwa na nchi.

Ufundi pia unahusu kuwepo kwa mifumo na utaratibu wa kutambua viwango vya usalama mtandaoni na mikakati mahsusi kwa shughuli hii.

Uwezo ni pamoja na kuwepo kwa kampeni za kuongeza uelewa na stadi za watu kwenye masuala ya mitandao. Nguzo hii inahusu pia kuwepo vivutio mbalimbali.

Ushirikiano ni pamoja na juhudi za ndani ya nchi za kujenga ubia wa ndani au kimataifa kuendeleza usalama mtandaoni.

Tanzania imepata asilimia 100 kwenye sheria, Mifumo na Ushirikiano; na asilimia 98 kwenye Ufundi na kujenga uwezo.

Baadhi ya vitu vilivyochangia kupaa kwa Tanzania kwenye CGI ya 2023 ni Sheria ya Ulinzi wa taarifa binafsi na kuwepo kwa kitengo cha dharura cha kitaifa cha kushughulikia masuala ya usalama wa mitandao Tanzania – CERT, ambacho kiko Mamlaka ya Mwasiliano Tanzania (TCRA).

Ushirikiano wa wadau wa ndani na wa nchi jirani na kimataifa pia umechangia kwa kiasi kikubwa kuiwezesha Tanzania kuwa juu.

Tanzania kupitia TCRA inatekeleza mpango wa kuhamasisha wavumbuzi kubuni bidhaa na huduma za kuongeza matumizi ya TEHAMA nchini ili kujenga uchumi wa kidijiti.

Nchi 15 kati ya 46 kwenye ngazi ya juu ya tathmini zimefungana kwa kuwa na pointi 20 na kushika nafasi ya kwanza; hivyo kuifanya Tanzania kuwa katika nafasi ya 10, kama inavyoonekana kwenye jedwali 4.

**Jedwali 2: Tanzania ilivyopimwa kwenye nguzo tano. Kiwango cha juu ni pointi 20.**

| Nguzo | Pointi | Asilimia |
|---|---|---|
| Sheria | 20 | 100 |
| Mipango ya kiufundi | 19.61 | 98.05 |
| Mfumo wa usimamizi | 20 | 100 |
| Ujenzi wa uwezo | 19.57 | 97.85 |
| Ushirikiano | 20 | 100 |
| **Wastani wa asilimia** | 99.18 | |

**Chati 1: Nafasi ya Tanzania miongoni mwa nchi tano za Afrika kwenye kundi la nchi 46 zinazoongoza duniani (pointi)**






Akizungumzia kupaa kwa Tanzania, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri K. Bakari amesema matokeo hayo yatachangia kuwezesha nchi kujiamini zaidi inavyokabili changamoto katika mitandao ya intaneti.

Dkt Bakari amewataka wataalamu wa masuala ya usalama mtandaoni kujisajili na kupata leseni ya TCRA.

Hii itawawezesha kujitangaza zaidi na kufungua maeneo mapya ya ushirikiano kwenye masuala ya usalama mtandaoni.

Amesisitiza azma ya TCRA kuendeleza usalama na uimara wa mitandao nchini. Taasisi yake itaendelea

**Jedwali 3: Nafasi ya Tanzania miongoni mwa nchi vinara duniani.**

A (Sheria), B (Ufundi), C (Mifumo), D (Uwezo), E (Ushirikiano)

| Na | Nchi | Nguzo na alama kati ya 20 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | A | B | C | D | E |
| 1 | Bahrain | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Denmark | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | France | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Indonesia | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Italy | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Mauritius | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Netherlands | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Portugal | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Qatar | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Saudi Arabia | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | South Korea | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Thailand | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | Turkiye | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | United Arab Emirates | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 1 | United Kingdom | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 |
| 2 | Malaysia | 20 | 20 | 18.82 | 20 | 20 |
| 3 | Egypt | 20 | 20 | 20 | 20 | 19.94 |
| 4 | USA | 20 | 20 | 20 | 19.88 | 20 |
| 5 | Spain | 20 | 20 | 20 | 19.77 | 20 |
| 6 | Vietnam | 20 | 20 | 20 | 19.74 | 20 |
| 7 | Ghana | 20 | 20 | 20 | 19.27 | 20 |
| 8 | Singapore | 20 | 20 | 20 | 18.86 | 20 |
| 9 | India | 20 | 20 | 18.49 | 20 | 20 |
| 10 | Tanzania | 20 | 19.61 | 20 | 19.57 | 20 |

kushirikiana na taasisi nyingine za kikanda na kimataifa.

Mazingira salama mtandaoni yatawezesha Watanzania kufikia malengo yao ya kiuchumi na ya uraia, ameongeza.

TCRA imezindua kampeni ya nchi nzima kuinua kiwango cha uelewa wa umma kuhusu fursa za mtandao wa intaneti na usalama wake.

Kwenye kampeni hiyo inayolenga maeneo mengi ya kulinda watumiaji, TCRA itatoa mbinu na maarifa ya usalama mtandaoni na njia za kujilinda dhidi ya ulaghai kupitia simu za mkononi.

Kampeni pia inahusisha namna ya kugundua maudhui mitandaoni yanayolenga kupotosha, na jinsi ya kugundua habari feki.

Walengwa watafundishwa pia njia za kutoa taarifa za uhalifu, kwa kupiga namba 15040 bila malipo.

Kampeni hiyo ya awamu mbili itatekelezwa kati ya Oktoba na Desemba 2024, na Januari na Machi 2025.

Dkt Bakari amesema TCRA pia itawataka watu binafsi na taasisi zaidi kutumia kikoa cha Tanzania kwenye tovuti zao na anwani za barua pepe.



> "Vilevile yatawezesha nchi kujenga na kuimarisha uwezo wake wa kutekeleza mipango yake kwenye usalama wa mitandao, ambao ni muhimu kwenye ujenzi wa uchumi wa kidijiti na wa bluu.
>
> **— Dkt. Jabiri K. Bakari**
>
> *Mkurugenzi Mkuu wa TCRA*

# Hatari za kumsajilia mtu laini ya simu

Na Mwandishi wetu

**Dondoo muhimu kutoka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Usajili wa Laini za Simu, 2023.**

Kusajili laini ya simu kwa niaba ya mtu mwingine huenda ikaonekana kama msaada wa kawaida, lakini ina athari kubwa zinazoweza kusababisha madhara makubwa.

Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Kuhusu Usajili wa Laini za Simu, 2023 zinaeleza umuhimu wa kufuata taratibu za usajili wa laini za simu kwa ukamilifu.

Kanuni hizi zinakataza kutumia kitambulisho cha mtu mwingine kusajili laini ya simu na kueleza hatari za kisheria, kifedha na zinazohusiana na faragha zinazoweza kujitokeza.

Moja ya masuala muhimu ni jukumu la kisheria linalohusiana na usajili wa laini ya simu. Kwa mujibu wa kanuni za mwaka 2023, kila laini ya simu lazima isajiliwe kwa kutumia alama za kibayometria za mtumiaji halisi.

Hii inamaanisha kwamba alama za vidole au data nyingine ya utambulisho ya mtu atakayekuwa akitumia laini hiyo lazima ziunganishwe moja kwa moja na laini ya simu.

Kusajili laini ya simu kwa kutumia kitambulisho chako kwa niaba ya mtu mwingine ni uvunjaji wa kanuni hizi moja kwa moja. Ukibainika, unaweza kukabiliana na adhabu, ikiwemo faini au kifungo.

Ukiukaji wa kanuni hizi, unaweza kusababisha utozwe faini ya hadi shilingi milioni 5 au TZS milioni 50 kwa kampuni na pia unaweza kuhukumiwa kifungo cha hadi miezi 12.

Jukumu la kisheria haliishii tu kwenye usajili. Unapomsajilia mtu mwingine laini ya simu, unachukua dhamana ya kisheria kwa matendo yote yanayo fanyika kwa kutumia laini hiyo.

Kama mtu huyo atatenda uhalifu kama vile utapeli au kufanya miamala haramu, vyombo vya dola vitafuatilia rekodi za usajili hadi kukufikia uliesajili laini husika.



Mtoa huduma atahusisha mawasiliano yote yanayo-fanyika kwa laini hiyo na kitambulisho chako na hivyo utawajibika kwa matumizi mabaya ya laini hiyo.

Hii inajumuisha uhalifu wa fedha kwa njia ya simu, wizi wa utambulisho na uhalifu wa mtandaoni ambao umekuwa ukitendwa katika miaka ya hivi karibuni kutokana na ujio wa teknolojia za kidijiti.

Mbali na hatari za kisheria, kumsajilia laini ya simu mtu mwingine pia kuna athari kubwa kwa faragha yako. Unaposajili laini ya simu ya mtu mwingine, data zako za kibayometria hutumika, ikiwamo alama za vidole au utambuzi wa sura, kulingana na mfumo unaotumika.

Data hizi ni za kipekee na zinalenga kukulinda wewe pamoja na mfumo wa mawasiliano dhidi ya udanganyifu. Hivyo basi, unaporuhusu mtu mwingine kutumia laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina lako, unahatarisha faragha ya data zako.

Endapo mtumiaji huyo atafanya shughuli zisizofaa au kutumia vibaya huduma za simu kama vile huduma za pesa kwa njia ya simu ni utambulisho wako ambao utawekwa wazi.

**Zaidi ya hayo, data zako binafsi zinaweza kutumiwa vibaya kwa namna ambayo huwezi kuidhibiti na hivyo kukuweka kwenye hatari ya wizi wa utambulisho au hasara ya kifedha.**

Shughuli za udanganyifu zinazohusisha laini za simu zimeongezeka na wahalifu mara nyingi wanatafuta njia za kukwepa sheria.

Njia moja inayotumika ni kuwashawishi watu kusajili laini za simu kwa niaba yao, kisha kutumia laini hizo kufanya shughuli za kihalifu

Kanuni za mwaka 2023 za usajili wa laini za simu zimeweka adhabu kali ili kuzuia udanganyifu na kuhakikisha kwamba usajili wote wa laini za simu unahusishwa na mtumiaji halali.

Hata hivyo, watu wanapopuuza sheria hizi kwa kusajili laini kwa wengine, wanatoa mianya ambayo wahalifu wanaweza kuitumia.

Ikiwa laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina lako inahusishwa na miamala ya udanganyifu, matokeo yake yanaweza kuwa mabaya.

Sio tu kwamba unaweza kukumbana na adhabu za kisheria, bali pia unaweza kupata hasara za kifedha kutokana na matumizi mabaya ya huduma za simu kama vile huduma za pesa kwa njia ya simu au kushiriki katika mipango ya utapeli.

Hatari nyingine kubwa ni kushindwa kufuatilia au kudhibiti shughuli zinazohusishwa na laini ya simu uliyomsajilia mtu mwingine. Unapomsajilia mtu mwingine laini ya simu, unapoteza uwezo wa kufuatilia jinsi namba hiyo inavyotumiwa. Iwe laini hiyo inatumiwa kwa shughuli halali au zisizo halali, bado unawajibika kwa matumizi yake.

Kanuni hizi zinahitaji watumiaji wote wa laini za simu kusajiliwa kibayometriki, kuhakikisha uwajibikaji na ulinzi wa mtandao wa mawasiliano.

Unaposajili laini kwa niaba ya mtu mwingine, unapuuza hatua hizi za ulinzi na hivyo kujiweka kwenye hatari.

Matendo yoyote yasiyo ya kimaadili au ya kihalifu yatakayofanyika kwa kutumia laini hiyo bado yatakuwa yakihusishwa nawe, hata kama hukujua au kushiriki moja kwa moja.

Ingawaje kusajili laini ya simu kwa niaba ya mtu mwingine huenda kumeonekana kama kitendo cha msaada, na cha kiungwana kwa kuzingatia mtindo wetu wa maisha ya kushirikiana, kinakuweka kwenye hatari kubwa.

Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Kuhusu Usajili wa Laini za Simu, 2023 zimewekwa ili kulinda watu kwa kuhakikisha kuwa kila laini ya simu inasajiliwa kwa mtumiaji halali kupitia utambulisho wa kibayometria.

Kutofuata sheria hizi kunaweza kusababisha uchukuliwaji wa hatua za kisheria, kukusababishia hasara ya kifedha na kuhatarisha faragha yako.

Ni muhimu kufuata sheria na kuepuka kuwasajilia laini za simu watu wengine ili kujilinda dhidi ya hatari zisizo za lazima. Ikilazimu kumsajilia mtu mwingine basi awe ni kijana ambae hajakidhi vigezo vya umri, au mtegemezi.

**Baki salama!**

Kanuni zinapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, (TCRA) kwa kuingia

*https://www.tcra.go.tz/documents/regulations*

**Au skani hapa kusoma zaidi kanuni hizi**

MATUKIO

# TCRA yapongezwa kwa kuwezesha teknolojia wezeshi

Na Mwandishi wetu

Baraza la Wawakilishi Zanzibar limeipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kuandaa mazingira bora ya kusambaa kwa teknolojia ya uzao wa tano wa mawasiliano ya simu za mkononi (5G).

Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ya Baraza hilo waliotembelea makao makuu ya TCRA Dar es Salaam hivi karibuni walisema teknolojia hiyo, inayowezesha mawasiliano ya intaneti kwa kasi zaidi, itafungua fursa kwenye maeneo mengi.



Hayo ni pamoja na utoaji huduma za biashara, kilimo, viwanda, uchukuzi, afya na elimu kwa njia ya mtandao, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma alisisitiza.

Mhe. Mwanaasha ameishukuru TCRA kwa jitihada zake zinazoendelea kuhakikisha kuwa miundombinu ya 5G inasambazwa kwa kasi na ufanisi zaidi.

Hadi Juni 2024 kulikuwa na minara 754 yenye vifaa vinavyowezesha 5G Tanzania. Mkoa wa mjini Magharibi una minara 37, na ni wa tatu kwa idadi. Dar Es Salaam inaongoza, ikiwa na minara 541, ikifuatiwa na Dodoma (41), Arusha (27) na Mwanza (23).

Teknolojia hiyo imeenea kijiografia asilimia 15 ya Tanzania na miongoni mwa watu kwa asilimia mbili.

Mhe. Mwanaasha pia aliipongeza TCRA kwa kusimamia ushindani wenye tija katika sekta ya mawasiliano. Usimamizi makini umewezesha kupunguza gharama za mawasiliano na kuongeza upatikanaji wa huduma bora kwa watumiaji kwa gharama nafuu.

Aliongeza kuwa Kamati yake imefurahishwa na ujenzi wa jengo jipya la TCRA Zanzibar.

Kamati hiyo imehimiza TCRA kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi bora ya mitandao.

> Katika ulimwengu wa sasa ambapo teknolojia ni sehemu ya maisha ya kila siku, ni muhimu kwa wananchi kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mitandao na matumizi yake kwa usalama. Elimu hii itasaidia kupunguza hatari za uhalifu mtandaoni na kuimarisha usalama wa watumiaji wa mitandao.
>
> **— Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**
>
> ***Mwenyekiti Kamati ya Bajeti, Baraza la Wawakilishi Zanzibar***

Kamati hiyo ya wajumbe wanane na makatibu wanne iliambatana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi SMZ Dkt. Mzee Mohamed Mndewa pamoja na maafisa wa wizara hiyo. Dkt. Mzee alishawahi kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi TCRA.

# Huduma zazidi kuimarika

Taarifa ya kila robo mwaka ya TCRA inawasilisha hali ya maeneo yote ya sekta ya mawasiliano Tanzania. Toleo la Julai hadi Septemba, lilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dkt Jabiri Bakari, linaonesha kukua kwa mitandao na huduma nyingi. Tunawasilisha vipengele vikuu vya taarifa hiyo.

## Teknolojia za kisasa zapandisha intaneti

Sekta ya mawasiliano Tanzania imeshuhudia maendeleo makubwa ndani ya miezi mitatu, yanayooneshwa na kuenea huduma zinazotumia teknolojia za kidijitali maeneo mengi nchini.

Teknolojia za mawasiliano ya mkononi zenye uwezo mkubwa wa intaneti zimewezesha watumiaji wengi kupata huduma za data ya kasi.

Dkt Bakari amesema asilimia ya kuenea kwa teknolojia na vifaa vya watumiaji miongoni mwa watu iliongezeka kwa kati ya pointi moja na tatu kati ya Juni na Septemba 2024.

Huduma zinazowezeshwa na teknolojia za juu zaidi pia zimeongeza kasi ya intaneti, zimewezesha mitandao kuimarika na kutoa huduma kwa ufanisi zaidi. Vilevile teknolojia zimeongeza ubora wa huduma, aliongeza.

Teknolojia za simu za mkononi uzao wa tatu (3G) zimezidi kuenea kwa watu, kutoka asilimia 89 hadi 90.1. Uzao wa nne (4G) umeenea zaidi kutoka asilimia 83 hadi 84.9 na wa tano (5G) kutoka asilimia 15 hadi 18.

Kijiografia, 4G imeenea asilimia 73.6, kutoka asilimia 73 na 4G kwa asilimia 70.2, kutoka asilimia 69. Uzao wa tano kijiografia umeenea asilimia 2.2 Septemba 2024, kutoka asilimia mbili (2) Juni mwaka huu.

Teknolojia hizi zinawezesha huduma za maongezi, ujumbe mfupi (meseji) na intaneti.

Teknolojia ya 5G, ambayo iliingia Tanzania mara ya kwanza 2022 ina kasi kubwa ya intaneti, inapunguza ucheleweshaji wa kusafirisha data na inaunganisha watumiaji na mitandao kwa ufanisi zaidi. Taarifa hiyo imeeleza kwamba simu zenye uwezo mkubwa, au simu janja zimeenea miongoni mwa watu kwa asilimia 33.85, kutoka asilimia 31.5 Juni 2024.

Simu janja zina programu tumizi changamani zaidi na zinawezesha intaneti ya kasi.

Watumiaji wa intaneti Tanzania wameongezeka kwa asilimia tano kati ya Julai na Septemba 2024 – kutoka milioni 39.3 hadi 41.4 milioni.

Watumiaji wanakokotolewa kutokana na laini za simu zilizotumika kupata huduma ya intaneti ndani ya miezi mitatu iliyotangulia, kwa kutumia teknolojia yoyote ile.

Hata hivyo huduma za intaneti zinapatikana zaidi kupitia vifaa vya mkononi na visivyo na waya.

Taarifa inaonesha asilimia 99.7 ya watumiaji wa intaneti walipitia teknolojia za vifaa vya mkononi.

Matumizi ya data yameongezeka kutoka wastani wa megabaiti (MB) **4.647** kwa mtumiaji Juni mwaka huu hadi MB **4.855** Septemba 2024.

Wastani wa kasi ya kupakia data kwa watumiaji wa vifaa vya mkononi vinavyowezesha intaneti ya kasi, unaopimwa kwa megabaiti moja kwa sekunde (Mbps), uliongezeka kutoka Mbps 11.4 Juni 2024 hadi 13.3 Septemba.

## Laini zaongezeka asilimia 80 ndani ya miaka sita

Laini milioni 80.7 zilikuwa zinatumika katika mitandao mitano ya simu za mkononi nchini kote Septemba 2024, ambapo milioni moja zilikuwa zinatumiwa kwa mawasiliano ya mashine kwa mashine.

Laini zilizosajiliwa ziliongezeka kwa asilimia 5.4 – kutoka milioni 76.6 hadi milioni 80.7 kipindi hicho.

Laini zimeongezeka kwa asilimia 80 kati ya Septemba 2019 na Septemba mwaka huu – kutoka 44,798,361 hadi 80,662,041.

Zilizosajiliwa hadi Septemba mwaka huu ni pamoja na 79,646,221 zinazotumika kwa mawasiliano kati ya watu na 1,015,820 zinazotumika kwa mawasiliano ya mashine zenyewe bila kuingiliwa na binadamu.

Juni 2024 kulikuwa na laini 75,588,006 kwa mawasiliano ya watu na 962,928 kwa mawasiliano ya mashine kwa mashine.

Kuongezeka kwa laini za mashine kunaashiria kuenea Tanzania kwa teknolojia za kidijiti zinazojiendesha zenyewe.

Kuwepo kwa laini za simu kuzidi idadi ya watu Tanzania kunatokana na watumiaji kuwa na zaidi ya laini moja ya simu kwa sababu na matumizi mbalimbali. Sensa ya watu na makazi Agosti 2022 ilithibitisha kwamba Tanzania ina watu milioni 61.7.

Laini zinahusisha idadi inayotumika na sio watu wanaotumia.

Taasisi ya GSMA, inayoshughulikia maslahi ya watoa huduma za simu za mkononi ulimwenguni, inaeleza kuwa watumiaji halisi wanapatikana kwa kuigawa idadi ya laini kwa 1.8. Huu ndio wastani wa watu kumiliki laini.

## Akaunti pesa kwa simu zaongezeka mara tatu

Akaunti za pesa kwa simu zimeongezeka kwa asilimia tano kati ya Julai na Septemba 2024 na kwa asilimia 157 kati ya 2019 na mwaka huu.

Akaunti 60,815,533 za pesa kwa simu za mkononi zilikuwa zinatumika Septemba mwaka huu kulinganisha na 58,140,257 Julai.

Akaunti hizi ni zile zilizotumika mitandaoni kwa huduma za kifedha na zilizofanya angalau muamala mmoja ndani ya miezi mitatu iliyotangulia.

Miamala ya pesa kwa simu iliongezeka kwa asilimia 9.9 kati ya Julai na Septemba. Hii inajumuisha pia idadi ya pesa zilizowekwa kwenye akaunti au kutumwa kutoka kwa akaunti ya mwenye laini ya simu ndani ya miezi mitatu iliyotangulia.

Taarifa pia inaonesha kuwa miamala ya pesa kwa simu iliongezeka kwa asilimia 75 kati ya 2019 na 2023.

Iliongezeka kutoka 3,021,142,958 iliofanywa kupitia



akaunti 25,864,318 hadi 5,273,086,154 iliofanywa na akaunti 52,875,12.

Kuongezeka huku ni sawa na kukua kwa asilimia 19 kila mwaka.

Kukua kwa huduma za pesa kwa simu na malipo kidijiti Tanzania kumetokana na muingiliano wa watoa huduma za pesa kielektroniki.

Muingiliano huu unamwezesha mteja wa kampuni ya simu kutumia akaunti yake ya pesa kwa simu kufanya miamala mbalimbali,ikiwa ni pamoja na kwenye mitandao mingine na benki.

Vilevile kukua huku kumechangiwa na ufanisi wa wasimamizi wawili - TCRA kwa upande wa mawasiliano na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa sekta ya fedha.

TCRA inatoa leseni kwa watoa huduma za simu za mkononi, ambao pia wanatoa huduma za pesa. Inawapatia namba za mawasiliano na misimbo inayotumika kwenye miamala.

BOT inasimamia masuala ya kifedha na inatoa leseni kwa watoa huduma za simu wa wengine ku-wawezesha kutoa huduma za kifedha.

## Huduma televisheni kidijitali zaidi kuimarika

Utangazaji Tanzania umeendelea kuimarika na mawimbi ya televisheni kijitali kwa mfumo wa ardhini (DTT) sasa yanafikia asilimia 58 ya watu.

Mawimbi ya DTT yanafika asilimia 33 ya nchi nzima kijiografia, kutoka asilimia 32 Juni mwaka huu.

Mfumo wa DTT ulianza kutumika Tanzania mwaka 2014 baada ya nchi kuanza kutumia mfumo wa utangazaji wa televisheni kidijitali.

Mfumo wa utangazaji wa setilaiti, unaofupishwa DTH, umeenea kwa asilimia 100 miongoni mwa watu, na pia nchi nzima kijiografia.

Mawimbi ya utangazaji wa redio ya FM yameenea kwa asilimia 78 miongoni mwa watu Septemba kulinganisha na asilimia 75.52 Juni mwaka huu. Yameenea kijiografia kwa asilimia 56.5 kutoka 49.94 kipindi hicho.

TCRA ilitoa leseni mpya 15 za maudhui ya utangazaji kati ya Julai na Septemba. Hizo ni pamoja na moja ya huduma za redio kimkoa, tano za redio kiwilaya na mbili za redio za jamii.

Vilevile ilitoa leseni tatu za televisheni ya kulipiwa kitaifa robo mwaka ya Julai-Septemba 2024.

Leseni nyingine zilizotolewa ni moja ya redio mtandao, moja ya watayarishaji na wachakataji wa maudhui ya kutolewa mitandaoni na mbili za blogu za habari na matukio yanayotolewa kwenye tovuti.

Hadi Septemba 2024, TCRA ilishatoa leseni za huduma mbalimbali za maudhui na idadi kwenye mabano kama ifuatavyo: redio (246) na televisheni zisizolipiwa (33), televisheni za waya (63).

Nyingine ni leseni za televisheni za kulipia (29), televisheni mtandao (210), redio mtandao (10), blogu za habari na matukio (66) na posta na usafirishaji vifurushi (146).

Taarifa inaonesha kupanda na kushuka kwa idadi ya watu wanaonunua huduma za televisheni kwa waya.

Waliongezeka kutoka 14,350 mwaka 2020 kufikia 19,739 mwaka 2021 na 22,295 mwaka uliofuata, kabla ya kushuka hadi 16,223 mwaka 2023.

Taarifa inaelezea kushuka huku kuwa kunatokana na wateja kuhamia mifumo mingine ya utangazaji wa televisheni.

## Mwanga mpya huduma za posta

Kuna dalili kwamba idadi ya vitu vinavyosafirishwa kimataifa kutoka Tanzania na mtoa huduma wa posta kitaifa inaongezeka licha ya kushuka kwa kiasi kikubwa kati yam waka 2019 na 2021.

Vitu vilivyosafirishwa na Shirika la Posta Tanzania (TPC) kwenda nje ya nchi viliongezeka kwa asilimia 74 kati ya mwaka 2021 na 2023.

Vitu 979,625 vilipostiwa kimataifa mwaka 2023 ikilinganishwa na vitu 564,528 mwaka 2021. Mwaka huo ulishuhudia kuanza kuongezeka kwa vitu kwenda nje baada ya kupungua miaka iliyotangulia.

Vitu 2,873,312 vilisafirishwa kimataifa mwaka 2019. Idadi hiyo ilipungua na kufikia 564,528 mwaka 2021.

Sekta ya posta ulimwenguni pote imekumbwa na changamoto zinazotokana na kuenea kwa kasi kwa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Hali hii imewapa watumiaji wa huduma za posta mbadala wa mawasiliano. Aidha, mawasiliano ya kielektroniki yameongeza ufanisi kwenye shughuli za watumiaji.

Janga la homa ya mapafu – UVIKO 19 pia limechangia kuzorota kwa huduma za posta. Hii ilitokana na kuvurugika kwa mifumo ya usafirishaji vitu vya posta.

Hata hivyo, watoa huduma wa posta wanatumia TEHAMA kwenye shughuli zao. Wengine wameanzisha huduma mbadala.

Dkt Bakari alisema hivi karibuni kwamba TCRA inahimiza watoa huduma wa posta na vifurushi kutumia teknolojia za kisasa zenye ufanisi.

Hizi ni pamoja na mifumo ya kidijiti na mifumo inayojiendesha yenyewe ambayo hurahisisha utendaji na kuboresha upatikanaji wa huduma za posta.

## Leseni zaidi huduma muhimu kidijiti

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imetoa leseni mpya 38 kwa makundi na aina tofauti za huduma na soko kati ya Julai na Septemba 2024, ikijumlisha sita kwa huduma zitakazoharakisha utekelezaji wa mikakati ya Tanzania kujenga uchumi wa kidijitali.

Leseni hizo sita mpya ni pamoja na za Miundombinu ya Mawasiliano, Huduma za Mawasiliano na ya Programu tumizi za Mawasiliano.

Leseni moja ni ya miundombinu ya mawasiliano. Hii inamruhusu mtoa huduma kumiliki miundombinu.

Aidha kuna nyingine ya Huduma za Mawasiliano, ambayo inamruhusu mwenye leseni kutoa huduma za msingi za kuunganisha mitandao mbalimbali ya mawasiliano.

Anaweza kutumia miundombinu yake au ya mwingine.

Leseni mpya nne zimetolewa kwa programu tumizi za mawasiliano. Hizi zinawaruhusu wamiliki kuwezesha matumizi ya huduma kama vile za data ambazo zinawezesha matumizi ya intaneti.

Watumiaji wa intaneti Tanzania yameongezeka kwa asilimia tano kati ya Julai na Septemba 2024, kutoka milioni 39.3 hadi milioni 41.1.

Watumiaji wanakokotolewa kutokana na laini za siku ziliotumika kupata huduma ya intaneti ndani ya miezi mitatu iliyotangulia, kwa kutumia teknolojia yoyote ile.

Serikali ina lengo la kuwezesha asilimia 80 ya watu Tanzania kupata huduma za intaneti ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025.

Kipindi hiki pia TCRA imeidhinisha vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki 184 kutumika Tanzania. Kanuni zinataka vifaa vinavyoingia nchini kuidhinishwa. TCRA inatoa leseni za uagizaji na usambazaji wa vifaa vya kielektroniki.

Leseni nyingine zilizotolewa robo mwaka huu ni moja ya redio kimkoa, tano za redio kiwilaya, mbili za redio za jamii na tatu za huduma za televisheni za kulipiwa kitaifa

Nyingine ni moja ya redio mtandao, moja ya kutoa huduma za kuandaa na kuchakata maudhui ya mtandaoni, na blogu za habari na matukio mbili.

Takwimu limbikizi zinaonesha kuwa kufikia Septemba 2024 TCRA ilikuwa imetoa leseni 35 za Miundombinu ya Mawasiliano, 16 za Huduma za Mawasiliano na 146 za watoa huduma za programu tumizi za mawasiliano.

Leseni nyingine za huduma zilizotolewa hadi sasa ni redio 246, huduma televisheni zisizolipiwa 33 na televisheni za waya 63. Aidha kuna televisheni za kulipia 29 televisheni mtandao 210 redio mtandao 10, blogu za habari na matukio 66 na watoa huduma za posta na usafirishaji vifurushi 146.

## Rukwa, Moro zavuma vibaya ulaghai mitandaoni

Mikoa ya Rukwa, Morogoro na Mbeya inaongoza kwa matukio yaliyoripotiwa ya ulaghai kupitia mitandao ya simu za mkononi Septemba 2014.

Wachambuzi wanasema hali hii inahujumu mikakati ya serikali kuendeleza ushirikishaji wa wananchi kwenye mifumo ya kifedha na kujenga uchumi wa kidijiti.

Wahalifu mitandaoni, wakiwemo matapeli kwenye mikoa hiyo wanawarubuni watumiaji wa na wakala wa pesa kwa simu hasa kwenye wilaya za Sumbawanga, Kilombero na Mbeya.

Taarifa hiyo, iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dkt Jabiri Bakari inasema matukio 16,002 ya ulaghai yameripotiwa Tanzania nzima, ambapo asilimia 77 ni kwenye mikoa hiyo mitatu.

Rukwa inaongoza kwa matukio 5,571 (asilimia 36), Morogoro 5,486 (asilimia 34) na Mbeya 1,112 (asilimia saba).

Taarifa inataja uhalifu unaofanyika kuwa ni pamoja na kubadilisha laini za simu za watumiaji bila ridhaa yao na kuwalaghai watu kutoa taarifa zao bila kutilia mashaka wanaozihitaji.

Taarifa hizi ni zinazohusu akaunti zao za pesa kwa simu au za kibenki, miamala, nywila na namba za siri. Hii inawawezesha wahalifu hao kuiba kwenye akaunti za simu, benki au za wakala wa huduma za pesa mtandao.

Uchambuzi wa taarifa hiyo unaonesha kuwa matukio yaliyoripotiwa Septemba yalikuwa machache kuliko ya Juni na Machi 2024. Matukio 17,319 yaliripotiwa Machi. Yaliongezeka kwa asilimia 57 na kufikia 22,257 Juni.

Dkt Bakari amewakumbusha wananchi na watumiaji wa mitandao na watoa huduma za pesa kupitia simu kuwa macho dhidi ya ulaghai mitandaoni.

Aidha wanatakiwa kupiga simu kwa msimbo 140 wanapokumbana na kadhia ya ulaghai.


TCRA inatekeleza mpango kabambe unaotekelezwa Tanzania nzima kwa awamu kuongeza uelewa wa watu kuhusu fursa za kidijiti na usalama mitandaoni.

Kampeni hiyo yenye awamu mbili inatekelezwa kati ya Oktoba na Desemba mwaka huu, na Januari na Machi 2025.


# Sekta ya Mawasiliano katika namba

## Tanzania yavunja rekodi idadi ya laini za simu zilizosajiliwa


### Idadi ya laini zilizotumika kupata huduma za intaneti




### Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma wa M2M





### Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma wa P2P





## Dondoo za Pesa Mtandao

### Idadi ya akaunti za pesa mtandao iliongezeka kwa 9% kati ya Juni na Septemba 2024




### Nani anaongoza soko?





## Idadi ya laini za intaneti yaongezeka kwa 5%

Idadi ya laini za intaneti iliongezeka kwa 5% ndani ya robo mwaka hadi **milioni 41.4** Septemba 2024

**99.7%** Sehemu kubwa au 99.7% ya laini za intaneti kwa **njia ya simu** (Mobile wireless) ikilinganishwa na aina nyingine za huduma ya intaneti

**Teknolojia ya 2G** inatumiwa zaidi baada ya kurekodi laini za intaneti **18,340,688** Septemba 2024

### Idadi ya laini za Intaneti kwa njia ya simu kwa kila mtoa huduma kufikia Septemba 2024 (Milioni)




Chanzo: Takwimu za TCRA za hali ya mawasiliano Tanzania kati ya Julai na Septemba 2024

# Zifahamu sekta ndogo za Utangazaji na posta

## Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kwa kila mtoa huduma

| | |
|---|---|
| Agape Associates Limited | 1,840 |
| Azam Media Limited | 1,356,664 |
| Basic Trasmissions Limited (Digitek) | 15,000 |
| Basic Trasmissions Limited (Continental) | 68,968 |
| Multichoice Tanzania Limited (DSTv) | 234,415 |
| Star Media Limited | 477,236 |
| Zuku | 21,687 |
| **Jumla ya visimbuzi (DTT & DTH)** | **2,175,810** |

**63%** Takriban visimbuzi **2 kati ya 3** vilivyolipiwa Septemba 2024 ni vya Azam Media

## Dondoo za televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya

Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya **iliongezeka kwa 2%** katika robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024

**18,820**
Juni 2024

**19,153**
Septemba 2024


**36%** Zaidi ya **theluthi moja** ya watumiaji wa televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya wapo **Shinyanga**, **Tabora** na **Mwanza**

## Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi kwa robo mwaka iliyoishia Septemba 2024

**495,521** Bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi kati ya Julai na Septemba 2024, ikiwa ni chini ya kiwango kilichotumwa kati ya Aprili na Juni mwaka huu kwa 10%

| Aina | Idadi |
|---|---|
| Barua | 166,590 |
| Vifurushi | 145,678 |
| Vipeto | 12,791 |
| Nyaraka | 169,415 |
| Mizigo | 1,047 |

## Majaribio ya ulaghai kwa mtoa huduma za simu kwa robo mwaka iliyoishia Septemba 2024




**76%** Robo tatu au majaribio ya ulaghai **3 kati ya 4** yaliyorekodiwa Septemba 2024 yalitokea **Rukwa**, **Morogoro** na **Mbeya**

Chanzo: Takwimu za TCRA za hali ya mawasiliano Tanzania kati ya Julai na Septemba 2024